

**Swali:** Toba maana yake nini?.. na je ina umuhimu gani kwetu?

---

**Jibu:** Neno “**Toba**” liinatokana na neno “**kutubu**”. Mtu anayetubu maana yake kafanya “**TOBA**”. Na kutubu maana yake ni “**kugeuka, kutoka katika njia uliyokuwa unaiendea**”.. Maana yake kama mtu ameshawishika kugeuka kutoka katika njia au mwenendo aliyokuwa anauendea kwa njia ya majuto na maombi ya kuomba msamaha kama njia hiyo ilikuwa ni kwanza kwa mwingine, mtu huyo anakuwa ametubu, au amefanya **TOBA**.

Kibiblia mtu aliyegeuka na kuiacha njia ya dhambi aliyokuwa anaiende na kuomba msamaha kwa Mungu wake aliyemkosea, basi mtu huyo anakuwa amefanya TOBA, na ndio hatua ya kwanza kabisa ya Mtu kumsogelea MUNGU, hakuna njia nyingine tofauti na hiyo!.

Injili ya Yohana Mbatizaji na ya **BWANA YESU** (*Mjumbe wa Agano jipya*) ilianza na Toba.

*Yohana 3:1 “Siku zile aliondokea Yohana Mbatizaji akihubiri katika nyika ya Uyahudi, na kusema,*

*2 TUBUNI; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia”.*

Mathayo 4:17 “Tokea wakati huo Yesu alianza kuhubiri, na kusema, TUBUNI; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia”.

Maana yake watu waageuke na kuacha *maisha ya kuabudu sanamu, waache maisha ya mauaji, waache maisha ya uzinzi na uasherati, waache maisha ya ulevi na utukanaji n.k..* kwasababu Ufalme wa mbinguni hautawapokea watu wa namna hiyo.

Lakini pia si kutubu tu, bali ni pamoja na **“KUZAA MATUNDA YAPATANAYO NA HIYO TOBA”**.. Maana yake baada ya kugeuka na kuacha dhambi, basi mwongofu huyo anapaswa ajifunze kuishi maisha yanayoendana na toba yake hiyo, maana yake asirudie tena machafu ya nyuma yatawale maisha yake.

*Luka 3:8 “Basi, toeni matunda yapatanayo na toba; wala msianze kusema mioyoni mwenu, Tunaye baba, ndiye Ibrahimu; kwa maana nawaambia ya kwamba katika mawe haya Mungu aweza kumwinulia Ibrahimu watoto”.*

Je na wewe umetubia dhambi zako na kumkaribisha YESU maishani mwako? Kama bado basi fungua hapa ufuatilizie sala hii ya **TOBA na KRISTO YESU** ataingia maishani mwako kwa Imani

**>>>KUONGOZWA SALA YA TOBA**

Maran atha!

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:

Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au

Piga namba hizi: +255789001312 au +255693036618

**Mafundisho mengine:**

**Ni lazima mtu aongozwe sala ya toba ili awe ameokoka?**

**AGIZO LA TOBA LINAENDANA NA UBATIZO!.**

**ALIPOKUWA ANGALI MBALI, BABA YAKE ALIMWONA.**

**TOBA IGUSAYO MOYO WA BWANA.**

**KAMA MTUMISHI WA MUNGU, TAFUTA MAARIFA KWA BIDII.**

**Rudi nyumbani**

Share on:

WhatsApp

Print this post